Uchumi na BIASHARA



Shamba la Kahawa la AVIV katika Kijiji cha Lipokela, Songea mkoani Ruvuma.

Shamba la AVIV lathibitisha kilimo ni biashara na ajira

Na Albano Midelo

JUA la asubuhi linapochomoza juu ya safu za milima ya Kijiji cha Lipokela wilayani Songea katika Mkoa wa Ruvuma, miale yake hugusa miti ya kahawa iliyonyooka mithili ya wanajeshi waliopangwa kwa nidhamu.

Hapa ndipo penye shamba la kimataifa la kahawa la Aviv Tanzania Limited lenye zaidi ya hekta 2,000.

Kati ya hizo, hekta 1,000 zikiwa tayari chini ya kahawa inayozalisha kwa kiwango cha kimataifa.

Ni shamba linaloonekana kuwa jibu la vitendo kwa ndoto ya Tanzania ya kufufua uchumi kupitia kilimo, ajira na fedha za kigeni.

Uzito wa kitaifa na kimataifa

Kampuni ya Aviv Tanzania Limited imejikita kuzalisha kahawa bora ya daraja la juu kwa soko la kimataifa.

Inaendelea uk.13



Wafanyakazi wa shamba la AVIV wakiwa na aliyekuwa Mbunge wa Peramiho, Jenista Mhagama (katikati).



Rais Samia Suluhu Hassan akiangalia kahawa alipolitembelea shamba la AVIV katika ziara yake mkoani Ruvuma, Septemba 2024.

Shamba la AVIV lathibitisha kilimo ni biashara na ajira

Inatoka Uk. 9

Meneja wa shamba hilo, Hamza Kassim anasema linachangia asilimia 4.5 ya kahawa yote inayozalishwa Tanzania. Takwimu hizo zinalipa shamba hilo uzito wa kipekee katika tasnia ya kahawa nchini.

Katika soko la kimataifa, kahawa ya AVIV imefanya Tanzania itajwe mara kwa mara kwa uzalishaji wa kahawa bora barani Afrika.

Meneja Msaidizi wa Kampuni ya Aviv Tanzania Limited, Muthana Maruvand anasema siri ya mafanikio ya shamba hilo ni uwekezaji kwenye miundombinu ya kisasa ya umwagiliaji, visima virefu, mifumo ya umwagiliaji kwa njia ya matone na utaalamu wa kimataifa wa uzalishaji na usindikaji.

Kwa mujibu wa takwimu za kampuni, AVIV inatoa ajira za kudumu 1,400 na ajira za msimu 5,000, huku wafanyakazi wake wakitoka mikoa mbalimbali ikiwemo Ruvuma na Mtwara. Zaidi ya asilimia 60 ya kahawa inayozalishwa shambani hapo huuzwa moja kwa moja nje ya nchi na hivyo, kuchangia taifa kupata fedha za kigeni na kupunguza utegemezi wa wauzaji wa kati.

Rais Samia; uthibitisho wa dira ya kitaifa

Septemba 2024, Rais Samia Suluhu Hassan alitembelea shamba hilo na kutoa kauli iliyotikisa tasnia ya kilimo.

Katika ziara hiyo anasema: “Mafanikio ya kilimo hayatokei kwa bahati mbaya, bali ni matokeo ya juhudi za kimkakati za serikali.”

Anasema uzalishaji wa kahawa nchini umeongezeka kutoka tani 65 hadi tani 85 ukiingiza zaidi ya Dola za Marekani milioni 250 kwa mwaka.

Aidha, anatoa maelekezo maalumu kwa uongozi wa shamba hilo kuelekeza uwajibikaji wa kijamii (CSR) katika uchimbaji wa visima vya umwagiliaji kwa wakulima wadogo ili maarifa na fursa ziwafikie wananchi wengi zaidi.

Kauli hiyo inaenda sambamba na ripoti za kitaifa zinazoonesha kuwa kwa miaka mitano iliyopita, sekta ya kahawa imekuwa miongoni mwa sekta za kilimo zinazokua kwa kasi huku ikisukumwa na sera za uwekezaji, masoko ya nje pamoja na mikakati ya kimfumo ya kuboresha mazao ya kimkakati.

Sera, sheria zinazobeba mapinduzi ya kahawa

Mafanikio katika mashamba makubwa kama AVIV yanapata mizizi yake kwenye sheria na sera za taifa.

Hizi ni pamoja na Sera ya Taifa ya Kilimo 2013 inayosisitiza kilimo cha kibiashara na ushirikishwaji wa sekta binafsi pamoja na Sheria ya Kahawa inayoratibu uzalishaji, ubora, usindikaji na biashara ya kahawa kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB).

Sheria ya Uwekezaji Tanzania iliboreshwa ili kuvutia uwekezaji wa kimkakati katika kilimo na kuondoa vikwazo vya masoko.

Aidha, Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kahawa 2021–2026 unalenga kuongeza uzalishaji, ubora na thamani ya kahawa katika masoko ya kimataifa.

Sheria hizo zimefungua milango kwa mashamba makubwa kuwekeza moja kwa moja, kusafirisha nje ya nchi na kushiriki kuboresha mnyororo wa thamani wa kahawa.

> “AVIV imenifundisha kazi ya kuvuna na kutunza kahawa kitaalamu. Kwa msimu mmoja napata kipato kinachosaidia familia kwa mwaka mzima. Sasa tunaona kilimo kinaweza kuwa ajira ya uhakika.”

Sauti za wananchi kuhusu zao la kahawa

Mkazi wa Kijiji cha Lipokela wilayani Songea, Sophia Komba anasema: “Miaka ya nyuma tulikuwa tunalima kahawa kwa kutegemea mvua. Ukame ukija, uzalishaji unashuka, bei inaporomoka na mwisho tunakata tamaa. Hatukuwa na visima wala maarifa ya umwagiliaji wa kisasa.”

Kwa upande wake, Dastan Hyera ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Liganga wilayani Songea anasema uwepo wa shamba la Aviv umeleta mafanikio makubwa kwa wananchi wa kijiji hicho.

Anasema nyumba zao zimepanda thamani na hivi sasa wanapangisha kwa wafanyakazi wa shamba hilo chumba kwa Sh 20,000 hadi 25,000.

“AVIV imenifundisha kazi ya kuvuna na kutunza kahawa kitaalamu. Kwa msimu mmoja napata kipato kinachosaidia familia kwa mwaka mzima. Sasa tunaona kilimo kinaweza kuwa ajira ya uhakika,” anasisitiza Hyera.

Mfanyabiashara wa kahawa wilayani Songea, John Luoga anasema: “Tunahitaji mashamba makubwa zaidi, lakini pia ushirikiano uwe mkubwa kwa wakulima wadogo.”

Anaongeza: “Visima viongezwe vijijini, kahawa yetu iuzwe nje ya nchi bila urasimu na hata vijana wafundishwe ujasiriamali wa kahawa.”

Mazao mapya, masoko mapya, thamani mpya

Mbali na kahawa, AVIV tayari imeanza kulima pilipili manga na kuuza nje tani mbili kwa mwaka huku ikilenga kufikia tani tatu.

Hatua hii inaifanya kampuni isiwe tu shamba la kahawa, bali pia kitovu cha mazao ya kimkakati yanayolipa soko la kimataifa ikiimarisha uchumi wa mkoa na taifa.

Mnyororo wa thamani wa kahawa

Uzalishaji mkubwa wa kibiashara katika hekta zaidi ya 1,000, ajira zaidi ya 6,400 kwa mwaka wakiwemo waajiriwa wa kudumu 1,400 na 5,000 wa msimu, ni miongoni mwa mambo yanayoifanya AVIV kuwa mfano wa vitendo wa sera ya kilimo cha kibiashara yanayoonesha kuwa, uwekezaji mkubwa katika kilimo unaweza kubadili maisha ya watu, uchumi wa mikoa na taswira ya nchi kimataifa.

Mambo mengine ni pamoja kuwapo mifumo ya kisasa ya umwagiliaji, uuzaji wa moja kwa moja nje ya nchi, kahawa bora inayotangaza jina la Tanzania kimataifa na maarifa yanayomwagika kwa wakulima wa jirani.

Haya yote yanaifanya AVIV kuwa mfano wa vitendo wa sera ya kilimo cha kibiashara, ikionesha kuwa uwekezaji mkubwa kwenye kilimo unaweza kubadili maisha ya watu, uchumi wa mikoa na taswira ya nchi kimataifa.

Shamba la kahawa Lipokela limethibitisha kuwa kahawa ni dira mpya ya uchumi wa kilimo.

Wakati Tanzania inahitaji mwelekeo zaidi wa mafanikio ya kilimo cha kibiashara, hekta 2,000 za AVIV Songea zinathibitisha kwa vitendo kuwa kilimo ni biashara.

Wadau mbalimbali wa kilimo na uchumi wanasisitiza wawekezaji wadogo na wakubwa kama AVIV wazidi kujitokeza kuwekeza katika sekta ya kilimo, maarifa yashushwe kwa wakulima wadogo, visima viongezwe, masoko yafunguliwe kwa weledi na vijana wabebeshwe ujuzi.

Tanzania inaweza kuongoza dunia kwa kahawa, si kwa ndoto, bali kwa mashamba ya vitendo kama AVIV.

Biashara ya chakula na madhira yanayowasibu mamalishe sokoni

Na Joseph Sabinus

SEPTEMBA 30, 2025 Chama cha Wanahabari Tanzania (TAMWA) kiliendesha mdahalo uliohusisha wanafunzi wa shule za msingi, sekondari, mamalishe, walimu, wanahabari, watetezi wa haki za binadamu na usawa wa kijinsia pamoja na maofisa wa ustawi wa jamii kuhusu mchango wa vyombo vya habari kukabili ukatili wa kijinsia.

Katika mdahalo huo, zinatajwa aina za ukatili wa kijinsia ukiwamo wa kimwili kama vipigo, kihisia kama matusi na udhalilishaji, kiuchumi na kijamii.

Kwa mujibu wa chapisho la Equality For Growth (EFG) liitwalo: ‘Ukatili Wa Kijinsia Na Haki Za Wanawake: Sauti Ya Mwanamke Sokoni,’ ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake ni kitendo cha kuumiza mwanamke kisaikolojia, kimwili na kiakili kwa kumnyanyasa kwa kumzuia, kukiuka au kumnyima haki zikiwamo fursa za kiuchumi kujiongezea kipato na kuchangia maendeleo.

Ripoti ya Takwimu za Unyanyasaji wa Kijinsia Tanzania ya Mwaka 2024 iliyotolewa Februari 2025 inasema wanawake ndio waathirika wakubwa wa ukatili.

Aidha, Ibara ya 20 na 21 ya Mkataba wa Itifaki ya Maputo zinahimiza kukomesha unyanyasaji, udhalilishaji na matendo ya kushusha hadhi kwa wanawake huku Azimio la Beijing la Masuala ya Jinsia la Mwaka 1995 likisisitiza kuimarisha wanawake kiuchumi na kuondoa umaskini.

Katika mdahalo huo, Mkuu wa Mawasiliano, Sera na Uchechemuzi wa Tamwa, Florence Majani anataja ukimya kama tatizo kubwa linalokwamisha vita dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Mmoja wa washiriki ambaye ni mjasiriamali wa kuuza chakula (mamalishe) katika soko lililopo Mwananyamala wilayani Kinondoni (jina linahifadhiwa), anasema baadhi ya wanaume sokoni wanatumia lugha chafu dhidi ya mamalishe wanaowahudumia.

Anasema: “Kinachouma sana ni wanaume kutukana mamalishe matusi yanayohusu maumbile wanapodai pesa baada ya kuwahudumia chakula…”

Kwa mujibu wa uchunguzi, baadhi ya maneno ya udhalilishaji dhidi ya mamalishe wanapokwenda kupata huduma ni pamoja na ‘Kuna chakula kizuri kama wewe?’

Katika Soko la Tazara lililopo kushoto mwa Barabara ya Mandela kutoka Daraja la Juu la Mfugale kuelekea Temeke, Dar es Salaam, eneo la matunda aina ya matikiti, HabariLEO linakumbana na kilio kama hicho kutoka kwa mamalishe.

“Biashara ya mamalishe ina msaada mkubwa kwa familia lakini ina changamoto nyingi,” anasema Nyanyama Masamaki (si jina halisi) na kuongeza: “Kama una roho nyepesi, ni rahisi kukata tamaa na kuacha…”

Akifafanua adha zilizowahi kumkumba, Nyanyama anasema: “Unamaliza biashara saa saba au saa nane mchana lakini hadi saa mbili usiku hujalipwa; mtu anakula kisha anasema ‘sina hela’, anaondoka huku akikutukana.”

Anaongeza: “Mwingine ana hela kabisa lakini anasema hawezi kuchenji Shilingi 10,000 kwa ajili ya Shilingi 2,000!… Wengi wanapoona watu wanakula, wanafikiri hatupati hasara lakini tunapata hasara sana ndiyo maana hatupigi hatua; kila siku tuko vilevile, lakini tutafanyaje.”

Wakati wa jioni wanawake hao huwa katika hatari ya kuguswa hovyo, kuibiwa au kuporwa wanapofunga biashara.

Nyanyama anaongeza: “Mteja mwingine unamdai malipo anasema hata nisipokulipa una hasara gani wanaume wapo ‘kibao’ utapata na zaidi ya hii… wanadhani tunauza vyakula na kuuza utu wetu… Au, unashangaa eti kwa kuwa wewe ni mamalishe, anakuja anataka akushike tu anavyotaka. Hapana, hiyo haikubaliki tuna heshima zetu.”

Anasema baadhi ya wateja wanaume huomba namba za simu kwa ajili ya kuagiza chakula, kisha wakazitumia kwa usumbufu wa ‘mambo ya hovyo’ hata usiku bila kujali kwamba mtu yupo na familia.

“Kibaya zaidi unakuta hata katoto ka miaka 18, 19 au 20 kama watoto wangu, nako kanashindwa kuniheshimu. Kwa kweli hilo linaniuma sana mpaka natamani kuacha hii kazi… utakubali wangapi!” Anasema.

“Usipokuwa makini ‘utamaliza soko’ maana mwingine anakuja na ahadi eti atakuletea wateja wapya wanaotoka mikoani,” anasisitiza.

Anaongeza: “Mwingine akigundua msimamo wako, anatangaza vibaya biashara ilikukuharibia usipate wateja…”

Nyanyama anasema: “Kikubwa ni elimu na sisi kupaza sauti zetu kukataa kudhalilishwa na tunashukuru katika hilo, uongozi wetu wa soko maana hauna mchezo, ukibainika unafanya mambo ya hovyo kwa wanawale unaonywa na ukiendelea, unafukuzwa… Tunaomba msimamo huo uendelee.”

Wakizungumza kwa pamoja ofisini kwao, Mwenyekiti wa Umoja wa Wauza Matikiti Tazara (UWAMATA), Charles Jumbe, Katibu wa Uwamata, Alfan Rashid na Mjumbe wa Uwamata, Abdallah Kabondo wanasema kinachofanywa na baadhi ya wateja wanaume hakikubaliki katika jamii inayojali haki na usawa.

“Mamalishe waendelee kusimamia kazi zao na kutoa taarifa kwa wanaofanya upuuzi kama huo, mamalishe ni kama dada, shangazi, mama au ndugu zetu wengine. Wanastahili heshima na ni watu muhimu kwa huduma zao humu sokoni…” anasema Rashid.

Jumbe yeye anasema: “Hata kama ni utani, utani lazima uwe na mipaka bila kudhalilisha wala kunyanyasa na kuathiri shughuli na hadhi ya mwingine…”

Katibu wa Soko la Tazara wilayani Temeke, Zenda Robert anakiri kuwapo tatizo kubwa la watu kuhudumiwa chakula mapema, mteja kupata pesa mapema lakini kwa makusudi akachelewa kulipia chakula alichokula.

Anasema: “Kweli wengine wanachelewa kulipwa na mabosi wao lakini hao ni wachache, ndiyo maana mamalishe anapoleta malalamiko na mtu akasema bosi wake hajamlipa namwambia twende kwa bosi wako, akisikia hivyo, anasema ngoja nilipe yaishe…”

Imebainika kuwa, wakati wa jioni wanawake hao huwa katika hatari ya kuguswa au kuibiwa wanapofunga biashara.

Awali, mmoja wa wateja aliyeomba asitajwe alisema wakati mwingine wanachelewa kulipwa ujira kwa kazi zao za siku.



Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk Rose Reuben (kushoto), Mkuu wa Huduma za Ustawi wa Jamii katika Jiji la Dar es Salaam, Waziri Nashiri (katikati) na Mwakilishi wa GIZ, Nora Loehr wakishirikiana kukata utepe kuashiria uzinduzi wa Mradi wa ‘Sauti Zetu’ Dar es Salaam, Novemba 14, 2025.

Mintarafu hoja hiyo Zenda anasema: “Hao ni wachache; wengi wenye kasumba hiyo pesa wanakuwa wanayo lakini mtu anakaa nayo tu. Hiyo inakwamisha hawa akina mama kibiashara.”

Zenda anapaza sauti: “Wanawake wanapofanyiwa ukatili, watoe taarifa katika mamlaka hata hapa sokoni waje; hatuna mchezo katika hili...”

Mteja wa soko hilo ambaye ni mchuuzi wa matunda mitaani, Anasima Mwakelenga anasema: “Mtu asipojiheshimu lazima umchukulie hatua maana wateja wa chakula ni wengi na sehemu za kuripoti udhalilishaji huo ni nyingi hata polisi kuna dawati...”

Anasima anasema katika huduma za mamalishe, wanaodhalilishwa zaidi ni wasaidizi wanaotumwa kutafuta wateja.

Kwa nyakati tofauti, anaungana na Zenda kusema hao kwa siku wanafanya takribani safari nne kwa mteja mmoja ikiwamo ya kwanza ya kutafuta oda za chakula.

“Akishapata oda, anapeleka chakula, anaambiwa arudi baadaye kuchukua pesa, akirudi anaambiwa bado na mara ya nne ndipo anaweza kupata hiyo pesa, au akazungushwazungushwa na mwisho kuambiwa leo sina hela,” anasema Anasima.

Balozi wa Amani Duniani, Dk Christina Onyango anawahimiza waathirika wa ukatili huo kuchukua hatua za kisheria hadi mwisho ili kutoa fundisho kwa wengine.

“Mamalishe watumie uongozi wa soko na madawati ya jinsia kupata haki zao za kufanya biashara na kupata malipo stahiki ili waendelee na shughuli zao halali,” anasema.

Balozi Onyango ambaye pia ni Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi, Kivule katika Wilaya ya Kipolisi Ilala, Dar es Salaam anasema: “Watumie uongozi wa soko ambao polisi kupitia madawati wamekuwa wakiwajengea uwezo kwa kuwapa mamalishe na viongozi elimu sokoni na hata katika hoteli.”

Vyanzo mbalimbali vinataja sababu za ukatili wa kijinsia kuwa ni pamoja na ukosefu wa uelewa wa haki za wanawake, mitazamo hasi ya kijamii dhidi ya wanawake, udhaifu wa mifumo ya malalamiko na ukosefu wa usalama na usimamizi mzuri katika masoko.

Mkurugenzi wa taasisi ya Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza anasema unyanyasaji na udhalilishaji wanaofanyiwa mamalishe unawaathiri vibaya kibiashara, kiuchumi, kijamii na kisaikolojia.

“Mtu anakula, anakwepa kulipa kisha anaondoka na deni huku akijua kuwa mamalishe wengine wanapata bidhaa kwa ‘malikauli’ kama unga, mchele, sukari, mkaa, mafuta, nyama na vingine ili akiuza leo, alipe na kuchukua bidhaa nyingine kesho sasa kufanya ukatili huo katika kuwalipa ni kuwaweka katika kipindi kigumu kibiashara na hata kuathiri familia zao.”

Anashauri kuwepo programu na mifumo maalumu kukomesha na kudhibiti aina zote za ukatili, unyanyasaji na udhalilishaji ukiwamo wa kijinsia wanaofanyiwa mamalishe katika mazingira kazi zao kwa kuwepo njia salama na rahisi za kutoa malalamiko.

Anasema, “Kuwepo programu maalumu kuhakikisha mamalishe wanasikilizwa haraka wanapotoa taarifa kuhusu madeni na udhalilishwaji na kwa kuwa ni suala la mtu mmojammoja, masoko yajenge mifumo inayowafanya wasilazimike kwenda polisi kwa kesi ya sahani ya wali…”

Anaongeza: “Uamuzi kuhusu mambo hayo hasa madeni usiwe katika ngazi kubwa labda eti hadi kwa mwenyekiti au katibu wa soko, bali kuwepo mfumo maalumu kusimamia haki za wajasiriamali hao wadogo”.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tamwa, Dk Rose Reuben anasema mamalishe hawana budi kupata elimu endelevu ya biashara na masoko sambamba na namna ya kujua, kuepuka na kupambana na ukatili wa kiuchumi, unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia.

“Elimu ya biashara na masoko itawasaidia kujua namna ya kubaini na kufanya biashara na wateja waaminifu bila kujali mwonekano wa mtu,” anasema Dk Rose.

Anahimiza mamalishe kufanya kazi zao kwa vikundi na umoja kwani licha ya kuongeza usalama wa biashara yao, mbinu hiyo pia itawasaidia kukuza na kulinda mitaji yao.

Wadau wanasisitiza kutolewe elimu zaidi kuhusu haki za binadamu na usawa wa kijinsia, kutunga na kutekeleza sera kali dhidi ya unyanyasaji pamoja na kuimarisha ulinzi na uwajibikaji wa wasimamizi wa masoko.

Oktoba 14, 2025 Tamwa kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) walizindua mradi uitwao ‘Sauti Zetu’ unaolenga kupaza sauti za wanawake na watoto na kuelimisha jamii kuhusu kupambana na ukatili wa kijinsia.

Mradi huo unatekelezwa Dar es Salaam (Kinondoni na Temeke), Dodoma (Chamwino na Bahi) na Tanga (Lushoto na Tanga Mjini).